



Simba Sports Club

P.O.Box: 15318 | Tel: +255 222183330 | Msimbazi / Mchikichi Street, Dar Es Salaam - Tanzania

Email: info@simbasports.co.tz | Website: www.simbasports.co.tz

KATIBA

YA

SIMBA SPORTS CLUB

TOLEO LA MWAKA 2018

YALIYOMO

SEHEMU YA I.....	1
MASHARTI YA JUMLA.....	1
Ibara ya 1: Muundo, Makao makuu na Ushiriki.....	1
Ibara ya 2: Malengo.....	2
Ibara ya 3: Bendera na Nembo.....	3
Ibara ya 4: Lugha Rasmi na kutofautiana kwa maana za matini.....	4
SEHEMU YA II.....	5
WANACHAMA.....	5
Ibara ya 5: Aina ya Wanachama.....	5
Ibara ya 6: Sifa za Mwanachama.....	5
Ibara ya 7: Utaratibu wa kupata hadhi ya uanachama.....	6
Ibara ya 8: Upatikanaji wa Uanachama na vipaumbele vya mwenye kupata stahiki.....	6
Ibara ya 9: Uamuzi wa Uanachama.....	7
Ibara ya 10: Muundo wa Wanachama.....	7
Ibara ya 11: Haki za Wanachama.....	8
Ibara ya 12: Wajibu wa Mwanachama.....	8
Ibara ya 13: Kusimamishwa Uanachama.....	10
Ibara ya 14: Kupoteza hadhi ya Uanachama.....	10
Ibara ya 15: Kujiuzulu Uanachama.....	11
Ibara ya 16: Kufukuzwa Uanachama.....	11
SEHEMU YA III.....	12
MUUNDO.....	12
Ibara ya 17: Orodha ya Vyombo vya Utendaji:.....	12
A. MKUTANO MKUU.....	12
Ibara ya 18: Ufafanuzi na Muundo.....	12
Ibara ya 19: Idadi na Mgawanyo wa Wajumbe.....	13
Ibara ya 20: Mamlaka ya Mkutano Mkuu.....	13
Ibara ya 21: Mkutano Mkuu wa Kawaida.....	14
Ibara ya 22: Ajenda ya Mkutano Mkuu wa Kawaida.....	14
Ibara ya 23: Mkutano Mkuu wa Dharura.....	15
Ibara ya 24: Akidi.....	16
Ibara ya 25: Uendeshaaji wa Mkutano Mkuu.....	16

Ibara ya 26: Maamuzi na uchaguzi	17
Ibara ya 27: Sifa za Wagombea.....	18
Ibara ya 28: Marekebisho ya Katiba na Kanuni.....	19
B. BODI YA WAKURUGENZI	20
Ibara ya 29: Muundo	20
Ibara ya 30: Muda wa Madaraka wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi	21
C. SEKRETARIETI	21
Ibara ya 31: Uanzishaji, Miundombinu na Kazi:.....	21
Ibara ya 32: Mkurugenzi wa wanachama na Mashabiki.....	22
D. VYOMBO VYA HAKI	23
Ibara ya 33: Dhana.....	23
Ibara ya 34: Hatua za Kinidhamu.....	24
Ibara ya 35: Kamati ya Nidhamu	24
Ibara ya 36: Kamati ya Maadili	25
E. KAMATI YA UCHAGUZI.....	26
Ibara ya 37: Uanzishaji, Kazi na Majukumu.....	26
F. BARAZA LA WADHAMINI	26
Ibara ya 38: Muundo na mamlaka.....	26
G. MATAWI YA SIMBA SPORTS CLUB NCHI NZIMA.....	27
Ibara ya 40:(1) Matawi ya SIMBA SPORTS CLUB na kazi zake:.....	27
SEHEMU YA IV.....	32
FEDHA.....	32
Ibara ya 41: Mwaka wa Fedha	32
Ibara ya 42: Mapato	32
Ibara ya 43: Matumizi.....	32
SEHEMU YA V.....	33
MIPANGO BINAFSI.....	33
Ibara ya 44: Sheria za Michezo wa Mpira wa Miguu.....	33
Ibara ya 45: Mwenendo wa Viongozi na Vyombo wa Klabu.....	33
Ibara ya 46: Kufukuzwa Uanachama	33
Ibara ya 47: Migogoro ya Kisheria.....	33
Ibara ya 48: Leseni kwa Vilabu (Club Licensing).....	34
SEHEMU YA VI.....	35
MASHARTI YA MUDA NA MWISHO.....	35

Ibara ya 49: Mipango ya Utendaji	35
Ibara ya 50: Masuala yasiyoelezwa katika Katiba.....	35
Ibara ya 51: Masharti ya Kutoa Huduma katika Kipindi cha Mpito...	35
Ibara ya 52: Kupitishwa na tarehe ya Kuanza kutumika.....	35
KANUNI ZA MKUTANO MKUU	36
Ibara ya 1: Wajumbe	36
Ibara ya 2: Mwenyekiti	36
Ibara ya 3: Wasimamizi	36
Ibara ya 4: Wakalimani	37
Ibara ya 5: Mijadala	37
Ibara ya 6: Mzungumzaji	37
Ibara ya 7: mapendekezo	37
Ibara ya 8: Hoja za Utaratibu wa kufunga Mjadala	37
Ibara ya 9: kura.....	38

TAFSIRI

Vifupisho vifuatavyo vinatumika kutafsiri yafuatayo:

"SSC"	Ni Simba Sports Club
"IDFA"	Ni Chama cha mpira wa Miguu cha Wilaya ya Ilala
"DRFA"	Ni Chama cha Mpira wa Miguu cha Mkoa wa Dar es Salaam
"TFF"	Ni Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania
"FIFA"	Ni Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani
"CAF"	Ni Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika
"CECAFA"	Ni Baraza la Vyama vya Mpira wa Miguu Afrika Mashariki
"CAS"	Ni Mahakama ya Usuluhishi wa Michezo
"AT"	NI Baraza la Usuluhishi
"IFAB"	Bodi ya Vyama vya Mpira wa Miguu Duniani, inayoidhinisha na kubadilisha sheria za Michezo za mpira wa Miguu
"Klabu za Ligi Kuu"	Maana yake ni Klabu ambazo zinashiriki katika Ligi Kuu ya Mpira wa Miguu inayotayarishwa na TFF
"Klabu Nyingine"	Maana yake ni Klabu Nyingine zinazoshiriki katika Mashindano yanayoaandaliwa na TFF, wanachama wa TFF au Chama cha Mpira wa Miguu cha Wilaya Husika
"Chama cha Mpira wa Miguu cha Wilaya"	Maana yake ni Chama cha Mpira wa Miguu kilichoundwa katika Wilaya ndani ya Wilaya ambayo ofisi za Simba Sports Club Company Limited zitakuakwa Mujibu wa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutambuliwa na DRFA na TFF.
"Mkutano Mkuu"	Maana yake ni Chombo chenye mamlaka ya Juu, cha kufanya maamuzi yote ya kikatiba na cha kutunga sheria cha Simba Sports Club na chenye mamlaka ya kuchagua viongozi wa Simba Sports Club
"Mkutano wa Viongozi wa Mikoa na Bodi ya Wakurugenzi ya Simba Sports Club Company Limited"	Maana yake ni chombo chenye mamlaka ya kuzungumzia, kujadili maendeleo ya klabu na kutoa mapendekezo mbalimbali ya uendeshaaji wa shughuli za kila siku za Klabu.

Mwenyekiti	Itamaanisha Mwenyekiti aliyechaguliwa kwa mujibu wa ibara ya 27(1) (a) ya Katiba hii.
Rais	Itamaanisha Rais wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba Sports Club Company Limited.
Sekretariat	Itamaanisha watumishi wa kuajiriwa wa SIMBA SPORTS CLUB kama walivyoainishwa katika ibara ya 31 ya Katiba hii.
Simba Sports Club Company Limited	Itamaanisha Simba Sports Club Company Limited ambayo inamilikiwa kati ya Simba Sports Club kupitia Simba Sports Club Holding Company Limited na Mo Simba Company Limited baada ya Simba Sports Club kufanya maridhio ya mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji na umiliki katika mkutano mkuu uliofanyika tarehe 20/8/2017.
Simba Sports Club Holding Company Limited	Itamaanisha kampuni isiyo ya kibiashara iliyoanzishwa na Simba Sports Club kwa madhumini ya kumiliki hisa za Simba Sports Club katika Simba Sports Club Company Limited.
Bodi ya wakurugenzi	Ni bodi ya wakurugenzi ya Simba Sports Club Company Limited.
Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi	Itamaanisha wajumbe nane (8) waliochaguliwa na kuteuliwa kwa mujibu wa Ibara ya 27 ya Katiba hii

SEHEMU YA I

MASHARTI YA JUMLA

Ibara ya 1: Muundo, Makao makuu na Ushiriki

- 1) Klabu itajulikana kama **SIMBA SPORTS CLUB**.
- 2) SIMBA SPORTS CLUB imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa ya mwaka 1967 na marekebisho namba 6 ya mwaka 1971.
- 3) Makao makuu ya SIMBA SPORTS CLUB yapo katika barabara ya Msimbazi, Kiwanja Na. 6 na 7, S.L.P. 15318, Dar es Salaam, Wilaya ya Ilala, mkoa wa Dar es Salaam. Yanaweza kuhamishiwa mahali pengine kwa uamuzi wa Bodi ya Wakurugenzi.
- 4) SIMBA SPORTS CLUB haifungamani na upande wowote kwa masuala ya Siasa na Dini. Inakataza aina zote za ubaguzi wa kisiasa, dini, jinsia, kabila au rangi.
- 5) Imeanzishwa kwa muda usio na kikomo.
- 6) SIMBA SPORTS CLUB ni Mwanachama wa TFF na ni mmiliki wa Hisa kwa asilimia hamsini na moja (51%) katika kampuni iitwayo Simba Sports Club Company Limited. Umiliki huo wa Hisa wa Simba Sports Club katika Simba Sports Club Company Limited ni kupitia kampuni iitwayo "Simba Sports Club Holding Company Limited" kampuni isiyojihusisha na masuala ya kibiashara. Kwa mantiki hiyo Simba Sports Club itaheshimu katiba, kanuni, maagizo na maamuzi ya TFF, CECAFA, CAF na FIFA na kuhakikisha kuwa yanaheshimiwa na wanachama wake.

Ibara ya 2: Malengo

1. Malengo ya Klabu:

a) Kumiliki hisa katika Simba Sports Club Company Limited, kampuni ambayo malengo yake ni: -

- (i) Kushiriki na kuendeleza mchezo wa mpira wa miguu ikiwa ni pamoja na kuanzisha vituo vya michezo ndani ya nchi.
- (ii) Kuwa mwanachama wa vyama vya michezo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kimataifa.
- (iii) Kuhamasisha michezo kwa ujumla, ikiwemo mpira wa miguu.
- (iv) Kukuza mchezo wa Mpira wa Miguu, kwa kutoa huduma na kusimamia timu za wachezaji wa mpira wa Miguu zenye jina la SIMBA SPORTS CLUB katika mashindano yoyote na Klabu nyingine ndani ya Tanzania na Kimataifa.
- (v) Kusajili wachezaji wa Mpira wa Miguu wa Ridhaa na wasio wa Ridhaa kuchezea timu ya SIMBA SPORTS CLUB.
- (vi) Kukuza na kuendeleza michezo katika jamii kwa ushirika wa moja kwa moja, ufadhili au usimamiaji wa timu za michezo mbalimbali.
- (vii) Kuanzisha, kushauri, kusaidia na kuendeleza matawi ya wapenzi wa SIMBA SPORTS CLUB katika ngazi ya Mikoa, Wilaya, Tarafa, Kata, Kijiji, Mtaa, Mashirika, Taasisi na mahala popote pale kwa idhini ya bodi ya wakurugenzi.

b) Fursa za Kijamii:

- i. Kuwa chombo ambacho wadau wenye tamaduni na itikadi sawa za kimichezo, watakusanyika pamoja, kutegeneza umoja kupitia mfumo wa uanachama, na kupitia umoja huo waweze kuunganisha nyenzo zao na kuwa wamiliki wa hisa katika kampuni ya Simba Sports Club Company Limited.
- ii. Kusaidia na kuchangia asasi zozote za hisani au umma, jumuiya, vyama au kikundi chochote.

c) Utawala:

Kuanzisha utawala ambao utaweza kusimamia maslahi mapana ya wanachama kwenye umiliki wao wa hisa katika Simba Sports Club Company Limited, kwa kutumia Mameneja na wafanyakazi waaajiriwa wenye ujuzi wa hali ya juu.

d) Fursa za Kihistoria, Kiutamaduni na Jamii:

Kukuza michezo kwakufanya utafiti wa maendeleo ya kijamii, kiutamaduni na kihistoria hasa Mpira wa Miguu hapa Tanzania.

e) Malengo Mengine Makuu na Madaraka:

Kuendeleza Mpira wa Miguu kwa kufanya mambo mengine ambayo ni muhimu na yatakayosaidia kufanikisha malengo yaliyotajwa hapo juu ikiwemo kuisaidia Simba Sports Club Company Limited kujiendesha kibiashara kwa kuongeza idadi ya wapenzi na kuhamasisha umoja wa wapenzi hao kujikusanya na kujiendesha kama chombo ili kuwa soko zuri la bidhaa za kampuni.

Ibara ya 3: Bendera na Nembo

- 1) SIMBA SPORTS CLUB itatumia Bendera yenye rangi nyekundu na nyeupe na Nembo iliyopitishwa na bodi ya wakurugenzi ya Simba Sports Club Company Limited. Rangi nyingine inaweza kuongezwa kutokana na matakwa ya kibiashara.

Ibara ya 4: Lugha Rasmi na kutofautiana kwa maana za matini

- 1) Lugha rasmi za SIMBA SPORTS CLUB ni Kiswahili au Kiingereza, nyaraka rasmi zote na matini zitaandikwa kwa lugha rasmi. Endapo kutakuwa na hitaji la tafsiri au mgongano wa tafsiri kati ya nyaraka ya lugha rasmi basi ile ya Kiswahili ndio itatumika kuondoa utata au mgongano huo.
- 2) Lugha ya Mkutano Mkuu itakuwa ni Kiswahili au kiingereza.
- 3) Itokeapo kutofautiana kokote katika tafsiri ya matini katika lugha tofauti, matini yaliyoandikwa kwa Kiswahili yatahesabiwa kuwa ndiyo yanayokubalika.

SEHEMU YA II

WANACHAMA

Ibara ya 5: Aina ya Wanachama

- 1) SIMBA SPORTS CLUB itakuwa na idadi ya wanachama isiyozidi 50,000 ambayo inaweza kuongezwa au kufanyiwa mabadiliko stahiki na Bodi ya wakurugenzi kutokana na sababu za lazima za uendesaji wa Klabu na umiliki wa hisa za Klabu katika Kampuni ya Simba Sports Club Company Limited.
- 2) Kutakuwa na aina zifuatazo za wanachama:

- i. **Wanachama kamili:** aina hii ya uanachama ikowazi kwa mtu yoyote anayetimiza masharti ya Ibara ya 6 na kukubaliwa na SIMBA SPORTS CLUB na atakuwa na haki ya kupiga kura na kuchaguliwa katika nyadhfa mbali mbali za uongozi wa klabu.
- ii. **Wanachama wa heshima:** Mwanachama ambaye ameitumikia klabu kwa muda mrefu na kutoa mchango mkubwa kwa SIMBA SPORTS CLUB. Pamoja na kuwa na haki zote za mwanachama kamili, hatalipa ada ya kila mwezi. Bodi ya Wakurugenzi itakuwa na mamlaka ya kumtunuku mwanachama yeyote kuwa mwanachama wa heshima.

Ibara ya 6: Sifa za Mwanachama

Uanachama utatolewa kwa Muombaji ambaye:

- a) Ana akili timamu
- b) Ana tabia nzuri
- c) Ni mwaminifu
- d) Awe na umri usiopungua miaka 18.

Ibara ya 7: Utaratibu wa kupata hadhi ya uanachama

- 1) Bodi ya Wakurugenzi ndiyo chombo chenye dhamana ya kutoa kadi za uanachama. Kadi hizo zitasainiwa na Rais, Mwenyekiti na Mwanachama mwenyewe.
- 2) Kila maombi ya uanachama wa SIMBA SPORTS CLUB yatawasilishwa kwa maandishi kwa Sekretarieti ya SIMBA SPORTS CLUB baada ya kupitia Tawi la SIMBA la mahali anapoishi.
- 3) Maombi yataambatanishwa na:
 - a) Fomu ya maombi iliyojazwa ipasavyo.
 - b) Ada ya maombi kuendana na thamani halisi ya hisa zinazomilikiwa na SIMBA SPORTS CLUB katika Simba Sports Club Company Limited au mtaji ambao SIMBA SPORTS CLUB inataka kuukusanya ili kununua hisa zaidi katika Simba Sports Club Company Limited.
 - c) Ada nyingine yoyote kama itakavyoamuliwa na Bodi ya Wakurugenzi.
 - d) Mwombaji uanachama itabidi adhaminiwe na wanachama hai.
 - e) Tamko linalosema kwamba anakubali kufuata katiba hii, kanuni na maagizo katika muundo wake wa sasa, na kutegemea mabadiliko ya baadaye na pia kanuni na maamuzi ya TFF, CAF na FIFA.
 - f) Tamko linalosema kwamba anatambua mamlaka ya Baraza la Usuluhishi kuhusiana na migogoro yote ya kisheria inayohusu masuala ya Mpira wa miguu.

Ibara ya 8: Upatikanaji wa Uanachama na vipaumbele vya mwenye kupata stahiki.

- 1) Mwanachama wa SIMBA SPORTS CLUB, anayo haki kwa wakati wowote ule kuitaarifu sekretarieti ya SIMBA SPORTS CLUB

kwa maandishi kama ana nia ya kujiuzulu uanachama wake ndani ya SIMBA SPORTS CLUB.

- 2) Endapo Mwanachama wa SIMBA SPORTS CLUB atatangaza kujiuzulu uanachama wake na kuuza hisa zake, atapewa kipaumbele cha uanachama wake kuchukuliwa na muombaji mpya wa uanachama, kama kuna nafasi za uanachama katika leja ya wanachama bado ziko wazi.
- 3) Pale inapotokea Mwanachama wa SIMBA SPORTS CLUB kafariki, msimamizi wa mirathi ya Mwanachama aliyetangulia mbele za haki atawajibika kuwasilisha nakala ya cheti cha kifo, ambapo stahiki za marehemu utawekwa sokoni na kupewa kipaumbele cha kuchukuliwa na muombaji mpya wa uanachama, kama kuna nafasi za uanachama katika leja ya uanachama bado ziko wazi.
- 4) Endapo leja ya wanachama itafikia ukomo wa kujaza nafasi zote 50,000 za wanachama kikatiba na Bodi ya Wakurugenzi haijafungua nafasi mpya, wanachama wapya wataweza kupata uanachama kwa wanachama hai waliojiuzulu uanachama wao, au kujaza nafasi za wanachama waliotangulia mbele za haki, stahiki zinazopatikana zitaenda moja kwa moja kwa wanachama waliojiuzulu nafasi zao au wasimamizi wa mirathi ya wanachama waliotangulia mbele za haki, isipokuwa maamuzi ya nani apewe nafasi ya kuziba nafasi hizo za uanachama yatabaki kuwa ya Bodi ya Wakurugenzi.

Ibara ya 9: Uamuzi wa Uanachama

Bodi ya Wakurugenzi ina mamlaka ya kuamua kuhusu maombi na hadhi ya uanachama.

Ibara ya 10: Muundo wa Wanachama

Wanachama wa SIMBA SPORTS CLUB wanaunganishwa katika muundo wa chombo cha kushirikisha, kinachofuata sheria za Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, alimradi ufuataji huo hautaathiri uanachama wa Simba Sports kwa TFF.

Ibara ya 11: Haki za Wanachama

- 1) Haki ya kujua agenda ya mkutano mkuu, kuitwa mkutanoni katika muda uliotajwa, kushiriki katika mkutano, na kupata taarifa kuhusiana na utendaji wa Simba Sports Club Company Limited na kutumia haki yao ya kupiga kura.
- 2) Haki ya kuarifiwa masuala ya SIMBA SPORTS CLUB na Simba Sports Club Company Limited, kupitia chombo rasmi cha SIMBA SPORTS CLUB.
- 3) Haki ya kuchaguliwa kuwa mjumbe wa kamati mbali mbali za Simba Sports Club Company Limited isipokuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi hawezi wakati huo huo kuwa mjumbe wa Chombo cha Haki cha Simba Sports Club Company Limited au Kamati ya uchaguzi.
- 4) Haki nyingine zote zinazotokana na Katiba hii au zile zinazotambuliwa na kanuni, maagizo na maamuzi ya TFF, CAF na FIFA.

Ibara ya 12: Wajibu wa Mwanachama

- 1) Kila Mwanachama wa SIMBA SPORTS CLUB atakuwa na wajibu ufuatao:
 - a) Kulipa kiasi cha fedha anachodaiwa na SIMBA SPORTS CLUB kwa njia ya michango na ada. Endapo atashindwa kulipa ada ya uanachama kwa kipindi cha miezi 12, mwanachama atasimamishwa uanachama wake. Bodi ya Wakurugenzi itapeleka mashauri ya wanachama walioshindwa kulipa ada kwa kipindi cha miezi 12 katika vyombo vya haki kwa hatua stahiki.

- b) Kutopeleka masuala ya mpira wa Miguu katika Mahakama ya kawaida ya sheria. Mwanachama atakayetafuta msaada katika mahakama ya kawaida ya sheria kuhusu mgogoro unaohusiana na katiba, kanuni, maagizo, uchaguzi au maamuzi ya SIMBA SPORTS CLUB na Simba Sport Club Company Limited atafukuzwa uanachama mara moja na Chombo husika cha Haki.
- c) Mwanachama atakayefukuzwa uanachama wake atapoteza stahiki zake zote katika umiliki wa hisa wa SIMBA SPORTS CLUB katika Simba Sports Club Company Limited.
- d) Kukubali kufuata katiba hii, kanuni, maagizo na uamuzi wa Simba Sport Club Company Limited, SIMBA SPORTS CLUB na TFF, CAF na FIFA.
- e) Kufuata sheria za mchezo wa Mpira wa Miguu zinazotolewa na IFAB (International Football Association Board).
- f) Kutumia kifungu cha katiba kinachoeleza bayana kuwa hatua zozote za kisheria zinazohitajika kuamua mgogoro unaokihusu au mmojawapo wa wanachama wake, na kuhusiana na katiba, kanuni, uchaguzi, maagizo na uamuzi wa SIMBA SPORTS CLUB, Simba Sports Club Company Limited na TFF lazima ziwe kwa mujibu wa mamlaka pekee ya vyombo vya haki na baraza la usuluhishi litakaloamua hatua za kisheria.
- g) Asiwe na uhusiano wowote wa kimichezo na wanachama waliosimamishwa au kufukuzwa.
- h) Kufuata masharti yaliyobainishwa katika ibara ya 6 katika kipindi chote cha uanachama wake.
- i) Kufuata misingi ya uaminifu, uadilifu na mwenendo mzuri wa kimichezo kama kuonyesha mchezo wa kiungwana, na Wajibu mwingine unaotokana na katiba hii au kanuni, maagizo na

uamuzi wa SIMBA SPORTS CLUB, Simba Sports Club Company Limited na TFF.

- j) Kuvikubali na kuvitambua vyombo vya haki vya Simba Sports Club Company Limited, TFF, FIFA, CAF na CAS na maamuzi yake.

Ibara ya 13: Kusimamishwa Uanachama

- 1) Uvunjaji wa katiba, kanuni, maagizo na maamuzi ya SIMBA SPORTS CLUB na Simba Sports Club Company Limited unaweza kusababisha kusimamishwa au kufukuzwa uanachama wa SIMBA SPORTS CLUB.
- 2) Kwa matukio ya kinidhamu na ya kimaadili au uvunjaji wowote wa Katiba hii, Bodi ya Wakurugenzi itayapeleka mashauri hayo kwenye kamati za Nidhamu au za Maadili za Simba Sports Club Company Limited ambavyo ndivyo vyombo vya Haki vitakavyokuwa na mamlaka ya kutoa adhabu juu ya mustakabali wa uanachama ikiwemo kusimamishwa au kufukuzwa uanachama wa SIMBA SPORTS CLUB.
- 3) Uamuzi wowote wa kusimamishwa una maana ya kupoteza haki na wajibu unaohusiana na hadhi ya mwanachama wakati usimamishwaji unaendelea, isipokuwa usimamishwaji huo hautaathiri stahiki za mwanachama katika umiliki wa hisa ndani ya Simba Sports Club Company Limited au haki ya mwanachama kuuza stahiki zake katika umiliki huo.

Ibara ya 14: Kupoteza hadhi ya Uanachama

- 1) Hadhi ya uanachama itakoma kwa:
 - a) Kujiuzulu uanachama.
 - b) Kufukuzwa.
 - c) Kufa.
 - d) Kutolipa ada ya uanachama kwa Muda wa miezi kumi na miwili (12) bila sababu ya msingi.

2) Kupoteza hadhi ya uanachama hakutamwondolea mwanachama madeni yake kwa SIMBA SPORTS CLUB au kwa wanachama wengine.

Ibara ya 15: Kujiuzulu Uanachama

Mwanachama anaweza kuwasilisha barua ya kujiuzulu uanachama kwa rejesta kwa Mkurugenzi wa Wanachama na Mashabiki wa SIMBA SPORTS CLUB. Mkurugenzi wa Wanachama na Mashabiki mara moja ataanza mchakato wa kutangaza upatikanaji wa uanachama wa mwanachama huyo kwa mwanachama mpya ambapo malipo ya uanachama mpya yatatumika kulipa stahiki za mwanachama aliyejiuzulu uanachama wake.

Ibara ya 16: Kufukuzwa Uanachama

Vyombo vya Haki vinaweza kumfukuza mwanachama kutokana na uvunjwaji wa Katiba, kanuni, Maagizo na Maamuzi ya SIMBA SPORTS CLUB na Simba Sports Club Company Limited.

SEHEMU YA III

MUUNDO

Ibara ya 17: Orodha ya Vyombo vya Utendaji:

- 1) SIMBA SPORTS CLUB itakuwa na vyombo vya utendaji vifuatavyo:
 - a) Mkutano Mkuu
 - b) Bodi ya Wakurugenzi
 - c) Sekretarieti
 - d) Vyombo vya Haki
 - e) Kamati ya Uchaguzi
 - f) Baraza la Wadhamini
 - g) Matawi, Uongozi wa Wilaya na Mikoa ya SIMBA SPORTS CLUB nchi nzima

A. MKUTANO MKUU

Ibara ya 18: Ufafanuzi na Muundo

- 1) Mkutano Mkuu ni mkutano ambao wanachama wote wa SIMBA SPORTS CLUB wanakutana. Mkutano Mkuu ulioitishwa kwa kufuata utaratibu ndio wenye mamlaka ya kufanya maamuzi.
- 2) Hali kadhalika, watakaoitwa katika Mkutano Mkuu kama washauri ni Wajumbe waalikwa walioteuliwa na Bodi ya Wakurugenzi.
- 3) Bodi ya Wakurugenzi itaamua kuhusu ushiriki wa wasiokuwa wanachama watakaohesabiwa kuwa ni washiriki waalikwa (third parties) katika Mkutano Mkuu. Hata hivyo, hawatakuwa na haki ya kupiga kura, ingawa wataombwa ushauri kwa idhini ya mwenyekiti wa Mkutano.

Ibara ya 19: Idadi na Mgawanyo wa Wajumbe

1) Mkutano Mkuu wa SIMBA SPORTS CLUB utaundwa na wajumbe wafuatao:

a) Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi - wenye haki ya kupiga kura

b) Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ambao sio wanachama wa SIMBA SPORTS CLUB lakini ni Wakurugenzi katika Simba Sports Club Company Limited wakitoka upande wa Muwekezaji- wasio na haki ya kupiga kura

c) Wanachama wote walio hai - wenye haki ya kupiga kura.

d) Wanachama wa heshima - wenye haki ya kupiga kura.

e) Wajumbe waalikwa - wasio na haki ya kupiga kura.

2) Kila Mwanachama rasmi katika mkutano Mkuu wa SIMBA SPORTS CLUB lazima awe na kadi halali ya uanachama. Sekretarieti ya SIMBA SPORTS CLUB itawataka wanachama kuonyesha kadi hiyo kwa uthibitisho na kujiorodhesha kushiriki katika mkutano mkuu.

Ibara ya 20: Mamlaka ya Mkutano Mkuu

Mkutano Mkuu utakuwa na Mamlaka yafuatayo:

1) Kupitisha au kurekebisha Katiba na kanuni na kusimamia matumizi yake.

2) Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano uliopita.

3) Kupokea bajeti ya mwaka ya shughuli na mipango ya Simba Sports Club na Simba Sports Club Company Limited.

4) Kupokea taarifa ya Chombo cha ukaguzi wa Fedha cha Simba Sports Club na Simba Sports Club Company Limited.

5) Kupokea taarifa ya shughuli za Bodi ya Wakurugenzi.

6) Kila miaka minne (4), kuchagua viongozi.

Ibara ya 21 Mkutano Mkuu wa Kawaida

- 1) Mkutano Mkuu wa Kawaida utaitishwa na Bodi ya Wakurugenzi mara moja kwa mwaka, yaani ndani ya siku 120 baada ya mwaka wa fedha. Mwaliko wa mkutano huo lazima upelekwe kwa wanachama angalau siku thelathini (30) kabla ya mkutano huo. Mwaliko huu utatolewa kupitia vyombo vya habari, ofisi za matawi na kwenye ubao wa Ofisi za Makao Makuu ya Klabu. Hesabu za mwaka wa fedha uliotangulia zitawasilishwa katika Mkutano wa Mwaka wa Wanachama wote.
- 2) Agenda ya Mkutano itataja mahali, tarehe na muda utakaopangwa na Bodi ya Wakurugenzi. Agenda, taarifa za kazi, bajeti, taarifa za hesabu na nyaraka nyingine zinazohusika zitapelekwa kwa wanachama angalau siku saba (7) kabla ya mkutano kupitia anuani za matawi yao. Kila mwanachama atakuwa na haki ya kuomba dondoo liingizwe katika ajenda alimradi Sekretarieti ya SIMBA SPORTS CLUB inapokea ombi hili angalau siku ishirini na moja (21) kabla ya Mkutano.

Ibara ya 22: Ajenda ya Mkutano Mkuu wa Kawaida.

Ajenda ya Mkutano Mkuu wa kawaida itajumuisha mambo yafuatayo ya Kikatiba

- a) Kuhakika idadi ya wanachama wanaohudhuria mkutano.
- b) Kuthibitisha ajenda.
- c) Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano uliopita.
- d) Yatokanayo na kumbukumbu za mkutano uliopita.
- e) Hotuba ya Mwenyekiti.
- f) Kupokea na kujadili taarifa ya utendaji kutoka Bodi ya Wakurugenzi.

- g) Kupokea taarifa ya hesabu za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliotangulia za Simba Sports Club na Simba Sports Club Company Limited.
- h) Kupokea bajeti ya mwaka ya shughuli na mipango ya Simba Sports Club na Simba Sports Club Company Limited.
- i) Uchaguzi wa nafasi zozote zilizo wazi za Simba Sports Club na Simba Sports Club Company Limited.
- j) Kupokea na kujadili mapendekezo ya marekebisho ya kanuni na katiba za SIMBA SPORTS CLUB.
- k) Kujadili mapendekezo yaliyowasilishwa na wanachama au Bodi ya Wakurugenzi.

Ibara ya 23: Mkutano Mkuu wa Dharura

- 1) Bodi ya Wakurugenzi inaweza kuitisha Mkutano Mkuu wa Dharura, kama itaona inafaa.
- 2) Endapo wanachama hai wasiopungua 1000 watajiorodhesha na kuwasilisha kimaandishi ombi kwa Mkurugenzi wa Wanachama na Mashabiki wa Simba Sports Club, Bodi ya Wakurugenzi itawajibika kuitisha mkutano Mkuu wa dharura katika kipindi kisichozidi siku thelathini (30) baada yakupokelewa kwa ombi.
- 3) Wito wa mkutano mkuu wa dharura hauna budi kupelekwa kwa wanachama kupitia matawi yao angalau siku 15 kabla ya mkutano.
- 4) Ajenda na nyaraka nyingine muhimu zitapelekwa kwa wanachama kupitia kwenye matawi angalau siku saba (7) kabla ya Mkutano.
- 5) Endapo Mkutano Mkuu wa dharura utaitishwa kwa juhudi za Bodi ya Wakurugenzi, basi Bodi ya Wakurugenzi itaandaa ajenda. Endapo utaitishwa kwa ombi la wanachama 1000, ajenda itakuwa na masuala yaliyopendekezwa na wanachama hao.

6) Ajenda ya wanachama haitobadilika kwa hali yoyote.

Ibara ya 24: Akidi

- 1) Maamuzi ya Mkutano Mkuu yatakuwa halali wakati watakapopitishwa kwa wingi wa kura (50%+1) za wanachama waliohudhuria wenye haki ya kupiga kura, bila kuathiri aya ya 2 ya ibara hii. Mkutano Mkuu utakuwa ni halali endapo utahudhuriwa na wanachama wasiopungua mia tano (500). Endapo idadi hiyo ya wanachama haitafikiwa basi mkutano mkuu utaendelea siku inayofuata hata kama idadi ya wanachama haitofikia mia tano.
- 2) Iwapo akidi haikutimia, Mkutano Mkuu utafanyika siku inayofuata kwa agenda zile zile. Katika Mkutano huo hakutahitajika akidi; isipokuwa kama kuna ajenda ya marekebisho ya Katiba ya SIMBA SPORTS CLUB, uteuzi wa Watendaji, kufukuzwa kwa Mjumbe Mmoja au Wengi katika chombo cha SIMBA SPORTS CLUB.

Ibara ya 25: Uendeshaaji wa Mkutano Mkuu

- 1) Mkutano Mkuu utaendesha na Mwenyekiti aliyechaguliwa kwa mujibu wa Ibara ya 27 (1) (a) ya katiba hii, Mwenyekiti asipokuwepo Bodi ya Wakurugenzi itachagua mjumbe mmoja kati ya wajumbe sita (6) wa bodi ya Wakurugenzi waliochaguliwa kwa mujibu wa Ibara ya 27 (1) (a) - (b) kuwa Mwenyekiti wa Mkutano.
- 2) Mkutano unaweza kuteua idadi ya kutosha ya waangalizi.
- 3) Wanachama watazungumza katika mkutano kwa kutumia lugha rasmi ya SIMBA SPORTS CLUB.
- 4) Mwenyekiti atakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mkutano unaendesha kama ulivyopangwa. Kwa hali hiyo, Mwenyekiti atakuwa anayo haki ya kukatiza hotuba za wanachama.

- 5) Mkurugenzi wa Wanachama na Mashabiki atatayarisha kumbukumbu za mkutano na kuwapelekea wanachama kupitia matawi yao katika kipindi cha mwezi mmoja baada ya mkutano.

Ibara ya 26: Maamuzi na uchaguzi

- 1) Mkutano Mkuu hautatoa uamuzi kwa suala lolote lisilokuwamo katika ajenda.
- 2) Kila mwanachama rasmi atakuwa na kura moja na hatawakilisha zaidi ya mjumbe mmoja.
- 3) Uchaguzi utafanywa kwa kura ya siri.
- 4) Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo katika Katiba, maamuzi ya Mkutano Mkuu yatafanywa kwa wingi wa kura zilizopigwa na wanachama rasmi.
- 5) Maamuzi ya Marekebisho yoyote ya ajenda katika Katiba na Kanuni, Mabadiliko yoyote ya ajenda ya Mkutano Mkuu wa Kawaida yatahitaji theluthi mbili (2/3) ya kura halali zilizopigwa na wanachama waliohudhuria na kutimiza akidi ya mkutano husika.
- 6) Karatasi za kura zilizoharibika, karatasi za kura zisizotumika, au aina nyingine zozote za kutokupiga kura zisizotumika, au aina nyingine zozote za kutopiga kura hazitoingizwa katika hesabu ya kura halali zilizopigwa.
- 7) Uchaguzi wa wajumbe watakwaiwakilisha Simba Sports Club kwenye bodi ya Wakurugenzi utafanywa na kuamriwa kwa wingi wa kura wa wanachama waliohudhuria wenye haki ya kupiga kura.
- 8) Mkutano Mkuu wa uchaguzi utachagua wajumbe sita watakwaiwakilisha Simba Sports Club katika Bodi ya Wakurugenzi, nafasi mojawapo angalau awe ni mjumbe mwanamke.
- 9) Maamuzi mengine yote ya wanachama yatafanywa kwa kunyoosha mikono. Uchaguzi utaendeshwa kwa utaratibu wa kura ya siri

kwa kutumia karatasi zilizotayarishwa kwa maelekezo ya Kamati ya Uchaguzi.

- 10) Kupiga kura kwa uwakilishi au barua hauruhusiwi.
- 11) Uamuzi unaofanywa na Mkutano Mkuu utanza kutumika mara moja isipokuwa kama mkutano unapanga tarehe nyingine au kuiachia uamuzi huo Kamati ya Uchaguzi.
- 12) Uchaguzi Mkuu utafanyika kila baada ya miaka minne (4) kufuatana na vipindi vya uongozi kwa kugombea kwa vipindi vya miaka minne minne.

Ibara ya 27: Sifa za Wagombea

1. Kutakuwa na wajumbe nane (8) watakaoiwakilisha Simba Sports Club katika Bodi ya wakurugenzi; sita (6) wa kuchaguliwa na wawili (2) wa kuteuliwa ambao kati yao: -
 - (a) Mjumbe mmoja atachaguliwa kama Mwenyekiti na ni lazima awe na taaluma kiwango cha chini cha elimu ya angalau shahada ya kwanza au sifa inayolingana na hapo kutoka Chuo Kikuu kinachotambulika na Taasisi ya Vyu Vikuu Tanzania (TCU).
 - (b) Mjumbe mmoja (1) lazima awe na taaluma kiwango cha chini cha elimu ya angalau shahada ya kwanza au sifa inayolingana na hapo kutoka Chuo Kikuu kinachotambulika na Taasisi ya Vyu Vikuu Tanzania (TCU).
 - (c) Wajumbe wengine wanne (4) wa kuchaguliwa waliobaki wanatakiwa kuwa na elimu isiyopungua kidato cha nne na angalau mjumbe mmoja wapo kati yao awe mwanamke.
 - (d) Wajumbe wawili (2) watateuliwa na Mwenyekiti kutoka miongoni mwa wanachama ambao ni lazima wawe na taaluma ya angalau kidato cha nne.

2. Mtu yeyote anayegombea nafasi yeyote ya SIMBA SPORTS CLUB hana budi kutimiza masharti yafuatayo:

- i. Awe na sifa zinazotakiwa kwa nafasi husika na amelipa ada ya uanachama kikamilifu tangu alipoanza uanachama.
- ii. Awe na kiwango cha chini cha elimu kama ilivyoainishwa katika ibara ya 27 (1) (a) (b) na (c).
- iii. Kiongozi wa kuchaguliwa atakaa madarakani kwa vipindi viwili tu vya kupiga kura kwa nafasi ya uongozi. Endapo atataka kurejea madarakani baada ya kutumikia vipindi viwili mfululizo, itabidi asubiri kwanza kupita kwa walau uchaguzi mkuu mmoja wa kikatiba.
- iv. Asiwe aliyewahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai kwa kuhukumiwa kifungo.
- v. Awe na umri angalau miaka 25.
- vi. Awe ametimiza angalau miaka mitatu ya uanachama.
- vii. Asiwe mwamuzi wa mchezo wa Mpira wa miguu anayefanya shughuli za uamuzi kwa kipindi hicho.
- viii. Mwanachama mwenye umri wa Miaka 65 na kuendelea hataruhusiwa kugombea.

Ibara ya 28: Marekebisho ya Katiba na Kanuni

- 1) Mkutano mkuu una jukumu la kurekebisha Katiba na Kanuni Kuu za Mkutano Mkuu.
- 2) Pendekezo lolote la Marekebisho ya Katiba halina budi kuwasilishwa na mwanachama/wanachama kwa Sekretarieti. Pendekezo linalowasilishwa na mwanachama ni halali, alimradi limeungwa mkono kwa maandishi na angalau wanachama wengine mia moja (100) na kupelekwa kwa Mkurugenzi wa Wanachama na Mashabiki siku 21 kabla ya Mkutano Mkuu.

- 3) Kwa kura inayohusu marekebisho ya katiba kuwa halali, lazima wanachama halali wanaostaili kupiga kura wawe zaidi ya nusu. (50%+1).
- 4) Pendekezo la marekebisho ya katiba litapitishwa endapo 2/3 ya wanachama wenye haki ya kupiga kura watakaopiga kura na watakubaliana nalo.
- 5) Pendekezo la marekebisho ya Kanuni zinazohusu Matumizi ya katiba na kanuni Kuu za Mkutano Mkuu, lazima ziwasilishwe kwa maandishi kwa Sekretarieti siku 21 kabla ya Mkutano.
- 6) Pendekezo la marekebisho ya matumizi ya katiba na kanuni Kuu za Mkutano Mkuu litapitishwa tu iwapozaidi ya nusu (50%+1) ya wanachama waliohudhuria na wanaostahili kupiga kura watakubaliana nalo.

B. BODI YA WAKURUGENZI

Ibara ya 29: Muundo

- 1) Klabu ya Simba itafanya kazi chini ya Bodi ya Wakurugenzi ya Simba Sports Club Company Limited;
- 2) Wajumbe saba waliochaguliwa na kuteuliwa kwa mujibu wa ibara ya 27 watakuwa wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi na watafanya kazi kwa mujibu wa kanuni zinazoongoza Bodi ya wakurugenzi zilizoidhinishwa na Simba Sports Club Company Limited.
- 3) Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi hawezi kuwa wakati huo huo Mjumbe wa Chombo cha haki cha Klabu ya Simba au Kamati ya Uchaguzi.
- 4) Mjumbe wa bodi ya Wakurugenzi aliyechaguliwa na kuteuliwa kwa mujibu wa ibara ya 27 ya katiba hii atakoma kuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi iwapo atatenda au kufanya mojawapo ya mambo yafuatayo:

- a) Kujiuzulu kwa maandishi na kuwasilisha barua yake ya kujiuzulu kwa Bodi ya Wakurugenzi.
- b) Hatahudhuria mikutano minne mfululizo ya kawaida ya Bodi ya Wakurugenzi bila sababu za msingi.
- c) Anashindwa kutekeleza majukumu ya mjumbe kutokana na kuumwa au sababu nyingine yoyote kwa kipindi cha miezi 12 mfululizo.
- d) Atapatikana na kosa la jinai na kuhukumiwa kufungwa bila mbadala wa faini
- e) Kufariki.

Ibara ya 30: Muda wa Madaraka wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi

- 1) Muda wa Madaraka na Mamlaka wa wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi waliochaguliwa na kuteuliwa kwa mujibu wa ibara ya 27 ya katiba hii utakuwa miaka minne (4). Kamati za muda (Interim Committes) hazitaruhusiwa.
- 2) Mamlaka ya wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi yanaweza kuongezwa muda na Mkutano mkuu kwa sababu maalum za msingi.
- 3) Endapo itatokea kuwa nafasi, yoyote ya Bodi ya Wakurugenzi kuwa wazi, katika Mkutano Mkuu wa kawaida unaofuata nafasi hizo zitajazwa kwa kuchaguliwa wajumbe wengine kwa kipindi kilichobaki cha Mamlaka.

C. SEKRETARIETI

Ibara ya 31: Uanzishaji, Miundombinu na Kazi:

- 1. Kutakuwa na Sekretarieti yenye muundo wa Ajira wa SIMBA SPORTS CLUB.

2. Wafanyakazi wote wa Sekretarieti watakuwa wa kuajiriwa na wataajirwa na Bodi ya Wakurugenzi.

3. Sekretarieti itaundwa na:

a) Mkurugenzi wa wanachama na mashabiki

b) Nafasi nyingine kama itakavyoamuliwa na Bodi ya Wakurugenzi

4. Sekretarieti itaongozwa na Mkurugenzi wa Wanachama na Mashabiki na kazi zake mahususi ni:

a) Utekelezaji wa maamuzi ya Mkutano Mkuu, Bodi ya Wakurugenzi na vyombo vingine vya Simba Sports Club Company Limited.

b) Kufanya matayarisho ya Mkutano Mkuu.

c) Kutayarisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu.

d) Kuhakikisha usimamizi mzuri na utunzaji wa rasilimali za SIMBA SPORTS CLUB.

e) Kushughulikia mawasiliano ya SIMBA SPORTS CLUB na kusimamia ofisi za SIMBA SPORTS CLUB.

f) Kutunza vitabu vya Hesabu za Fedha za SIMBA SPORTS CLUB.

g) Kushughulikia mahusiano ya SIMBA SPORTS CLUB, wanachama wake na wadau wengine.

Ibara ya 32: Mkurugenzi wa wanachama na Mashabiki

Kutakuwa na Mkurugenzi wa wanachama na Mashabiki SIMBA SPORTS CLUB atakayesimamia Sekretarieti ya SIMBA SPORTS CLUB.

1) Mkurugenzi wa wanachama na Mashabiki atafanya kazi chini ya usimamizi na muongozo wa Mtendaji mkuu wa Simba Sports Club Company Limited.

- 2) Mkurugenzi wa wanachama na Mashabiki atakuwa Mwandishi wa Mkutano Mkuu na kuzihifadhi kumbukumbu hizo.
- 3) Mkurugenzi wa wanachama na Mashabiki atawasimamia wafanyakazi wa SIMBA SPORTS CLUB na Utendaji wa Sekretarieti.
- 4) Mkurugenzi wa wanachama na Mashabiki atakuwa Ofisa Masuhuli wa Klabu.
- 5) Mkurugenzi wa wanachama na Mashabiki atapokea mipango na bajeti, za kila mwaka kutoka Simba Sports Club Company Limited na kusimamia utekelezaji wake.

D. VYOMBO VYA HAKI

Ibara ya 33: Dhana

- 1) Simba Sports Club itatumia vyombo vya haki vya Simba Sports Club na Simba Sports Club Company Limited.
- 2) Vyombo vya haki vitakuwa ni Kamati ya Nidhamu na Kamati ya Maadili. Vyombo hivi vitakuwa huru na maamuzi yake hayataingiliwa na chombo chochote cha SIMBA SPORTS CLUB.
- 3) Bila kuathiri maeneo ya mamlaka yaliyoandaliwa na Mkutano Mkuu, vyombo vilivyotajwa hapo juu vinaidhinishwa kuchukua hatua mbalimbali za nidhamu na maadili zilizotajwa katika Katiba hii na Kanuni zinazohusika.
- 4) Muundo, maeneo ya mamlaka, na kazi za vyombo vya haki, vitakuwa kwa mujibu wa Kanuni mahususi ambazo lazima ziidhinishwe na Bodi ya Wakurugenzi.
- 5) Wajumbe wa vyombo vya haki watateuliwa na Bodi ya Wakurugenzi.

Ibara ya 34: Hatua za Kinidhamu

- 1) Onyo
- 2) Karipio
- 3) Kurudisha tuzo
- 4) Kusimamishwa
- 5) Kufukuzwa
- 6) Bodi ya Wakurugenzi itaandaa kanuni za nidhamu na za Maadili. pasipokuwa na kanuni za nidhamu na za Maadili za Simba Sports Club Company Limited, Kanuni za nidhamu na za Maadili za TFF au FIFA zitatumika

Ibara ya 35: Kamati ya Nidhamu

- 1) SIMBA SPORTS CLUB inatambua Kamati ya Nidhamu ya Simba Sports Club Company Limited, itakayokuwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe watatu watakaoteuliwa na Bodi ya Wakurugenzi, Mwenyekiti na Makamu wa Mwenyekiti lazima wawe na Taaluma ya Sheria.
- 2) Chombo hiki kitasimamia Katiba ya SIMBA SPORTS CLUB kwa kutumia kanuni zake za Nidhamu au kanuni za TFF pale ambapo kanuni za Nidhamu za Simba Sports Club Company Limited hazipo.
- 3) Kamati itapitisha uamuzi iwapo angalau wajumbe watatu wamehudhuria mmojawapo akiwa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti.
- 4) Kamati inaweza kutangaza hatua za kinidhamu zilivyoielezwa katika Katiba hii au kanuni zilizotayarishwa kutokana na Katiba hii dhidi ya Wanachama, Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi waliochaguliwa kwa mujibu wa ibara ya 26 (8) au Wafanyakazi wa SIMBA SPORTS CLUB.

- 5) Rufaa yoyote dhidi ya uamuzi wa Kamati ya Nidhamu ya Simba Sports Club Company Limited itapelekwa kwa kamati ya rufaa ya nidhamu ya TFF. Rufaa dhidi ya Maamuzi ya TFF yanaweza pia kukatiwa rufaa CAS ambayo itakuwa na maamuzi ya mwisho.

Ibara ya 36: Kamati ya Maadili

- 1) SIMBA SPORTS CLUB inatambua Kamati ya Maadili ya Simba Sports Club Company Limited, itakayokuwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe watatu watakaoteuliwa na Bodi ya Wakurugenzi. Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa kamati ya Maadili lazima wawe na taaluma ya sheria.
- 2) Chombo hiki kitasimamia Katiba ya SIMBA SPORTS CLUB kwa kutumia kanuni zake za Maadili au kanuni za TFF pale ambapo kanuni za Maadili za Simba Sports Club Company Limited hazipo.
- 3) Kamati itapitisha uamuzi iwapo angalau wajumbe watatu wamehudhuria mmojawapo akiwa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti.
- 4) Kamati inaweza kutangaza hatua za kimaadili zilizvoelezwa katika Katiba hii au kanuni zilizotayarishwa kutokana na Katiba hii dhidi ya Wanachama, Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi waliochaguliwa kwa mujibu wa ibara ya 26 (8) au Wafanyakazi wa SIMBA SPORTS CLUB.
- 5) Rufaa yoyote dhidi ya uamuzi wa Kamati ya Maadili ya Simba Sports Club Company Limited itapelewa kwa Kamati ya rufaa ya Maadili ya TFF. Rufaa dhidi ya Maamuzi ya Kamati ya Rufaa ya Maadili ya TFF yanaweza pia kukatiwa rufaa CAS ambayo itakuwa na maamuzi ya mwisho.

E. KAMATI YA UCHAGUZI

Ibara ya 37: Uanzishaji, Kazi na Majukumu

1. Kutakuwa na Kamati ya Uchaguzi wa SIMBA SPORTS CLUB itakayoteuliwa na Bodi ya Wakurugenzi, ambayo itahusika na kuandaa na kusimamia Uchaguzi wa SIMBA SPORTS CLUB, itaishauri Bodi ya Wakurugenzi kuhusiana na kanuni za uchaguzi. Kamati ya Uchaguzi ya SIMBA SPORTS CLUB itafanya kazi chini ya usimamizi na maelekezo ya Kamati ya Uchaguzi ya TFF.
2. Kamati ya Uchaguzi itaundwa na Mwenyekiti, Makamu wa Mwenyekiti na wajumbe watatu. Mwenyekiti na Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi lazima wawe na taaluma ya Sheria.
3. Kamati ya Uchaguzi ya SIMBA SPORTS CLUB itatekeleza majukumu yake kwa kutumia kanuni za uchaguzi za SIMBA SPORTS CLUB na kama hazipo kanuni za Uchaguzi za TFF zitatumika.
4. Kamati ya Uchaguzi ya SIMBA SPORTS CLUB itapitisha maamuzi iwapo angalau wajumbe watatu wamehudhuria mmoja wapo akiwa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti.
5. Maamuzi ya kamati ya Uchaguzi ya SIMBA SPORTS CLUB yanaweza kukatiwa rufaa kwa Kamati ya Rufaa ya Uchaguzi ya TFF ambayo maamuzi yake yatakuwa ya Mwisho.

F. BARAZA LA WADHAMINI

Ibara ya 38: Muundo na mamlaka

- 1) SIMBA SPORTS CLUB itakuwa na Baraza la Wadhamini litakalokuwa na wajumbe wanne (4) na ndiyo watakuwa wasimamizi na wadhibiti wa mali zote za Klabu zinazohamishika na zisizohamishika na watunzaji wa "LAKIRI" (SEAL) ya Klabu.

- 2) Wajumbe wa Baraza la Wadhamini watateuliwa na Bodi ya Wakurugenzi na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu na kuanza kazi mara watakaposajiliwa na Kabidhi Wasihi mkuu wa Serikali. Mkutano Mkuu ndio utakuwa na mamlaka ya kumuondoa mjumbe/wajumbe wa Baraza la Wadhamini toka kwenye wadhifa huo baada ya kupata taarifa toka Bodi ya Wakurugenzi.
- 3) Wajumbe wa baraza la wadhamini ndio watakua wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba Sports Club Holding Company Limited.
- 4) Baraza la Wadhamini litamiliki 99% ya hisa za Simba Sports Club Holding Company Limited kwa niaba ya SIMBA SPORTS CLUB na mwenyekiti wa baraza la wadhamini atamiliki 1% ya hisa za Simba Sports Club Holding Company Limited kwa niaba ya SIMBA SPORTS CLUB.

Ibara ya 39: Ukomo wa Wadhamini.

- a) Kufa, Kujiuzulu, Kupata maradhi ya akili, kufungwa jela/magereza.
- b) Kuvuliwa nyadhfa na mkutano Mkuu.
- c) Bodi ya Wakurugenzi itawasilisha katika mkutano mkuu pendekezo la kumuondoa/kuwaondoa wadhamini watakaobainika ni chanzo cha migogoro ndani ya Klabu, au kama Bodi ya Wakurugenzi itakavyoona inafaa vinginevyo kwa maslahi ya Klabu.

G. MATAWI YA SIMBA SPORTS CLUB NCHI NZIMA

Ibara ya 40: (1) Matawi ya SIMBA SPORTS CLUB na kazi zake:

- a) Kutakuwa na uongozi wa Matawi, Wilaya na Mikoa nchi nzima.
- b) Matawi yote ya SIMBA SPORTS CLUB watalipa ada ya uanachama kila mwaka kwa kiwango kitakachopitishwa na

Mkutano Mkuu baada ya mapendekezo ya Bodi ya Wakurugenzi.

c) Kila tawi litaruhusiwa kuwa na wanachama hai wasiozidi 250 na wasiopungua 50.

d) Kila tawi litafanya uchaguzi wa uongozi wake utakaohusisha Mwenyekiti wa Tawi, Makamu Mwenyekiti wa Tawi, Katibu Mkuu wa Tawi, Mweka Hazina wa Tawi na Wajumbe Watatu (3) (mmoja kati yao mjumbe mwanamke) ambao kwa ujumla wao ndio wataunda Kamati ya Utendaji ya tawi.

e) Mgombea wa nafasi yoyote ya Tawi atatakiwa kuwa na sifa zifuatazo: -

(i) Awe na sifa zinazotakiwa kwa nafasi husika na amelipa ada ya uanachama kikamilifu tangu alipoanza uanachama.

(ii) Uanachama wake uwe kupitia tawi husika.

(iii) Kiongozi wa kuchaguliwa atakaa madarakani kwa vipindi viwili tu vya kupiga kura kwa nafasi ya uongozi. Endapo atataka kurejea madarakani baada ya kutumikia vipindi viwili mfululizo, itabidi asubiri kwanza kupita kwa walau uchaguzi mkuu mmoja wa kikatiba.

(iv) Asiwe aliyewahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai kwa kuhukumiwa kifungo.

(v) Awe na umri angalau miaka 25.

(vi) Asiwe mwamuzi wa mchezo wa Mpira wa miguu anayefanya shughuli za uamuzi kwa kipindi hicho.

h) Matawi yatathibitisha uombaji wa wanachama wapya.

- i) Matawi yatashauri uongozi wa wilaya na mkoa husika pamoja na makao makuu kuhusu maendeleo ya klabu.
- j) Kila Tawi la SIMBA SPORTS CLUB ni lazima lisajiliwe na uongozi wa wilaya husika na litakuwa na namba yake ya usajili itakayotambuliwa katika mkoa husika na makao makuu.
- k) Kata Moja inaweza kuwana tawi zaidi ya moja la Simba Sports Club alimradi idadi ya wanachama wake walio hai katika tawi isizidi 250 na isipungue 50.

2. Muundo wa Uongozi wa Wilaya na Mikoa:

- a) Kila wilaya itafanya uchaguzi wa uongozi wake utakaohusisha Mwenyekiti wa Wilaya, Makamu Mwenyekiti wa Wilaya, Katibu Mkuu wa Wilaya, Mweka Hazina wa Wilaya na Wajumbe Watatu (3) (mmoja kati yao mjumbe mwanamke) ambao kwa ujumla wao ndio wataunda Kamati ya Utendaji ya wilaya.
- b) Mgombea wa nafasi yoyote ya Wilaya atatakiwa kuwa na sifa zifuatazo: -
 - (i) Awe na sifa zinazotakiwa kwa nafasi husika na amelipa ada ya uanachama kikamilifu tangu alipoanza uanachama.
 - (ii) Uanachama wake uwe ni kupitia moja ya tawi la wilaya husika.
 - (iii) Awe na kiwango cha chini cha elimu ya angalau kidato cha nne.
 - (iv) Kiongozi wa kuchaguliwa atakaa madarakani kwa vipindi viwili tu vya kupiga kura kwa nafasi ya uongozi. Endapo atataka kurejea madarakani baada ya kutumikia vipindi viwili mfululizo, itabidi

asubiri kwanza kupita kwa walau uchaguzi mkuu mmoja wa kikatiba.

(v) Asiwe aliyewahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai kwa kuhukumiwa kifungo.

(vi) Awe na umri angalau miaka 25.

(vii) Asiwe mwamuzi wa mchezo wa Mpira wa miguu anayefanya shughuli za uamuzi kwa kipindi hicho.

c) Wapiga kura wa kuchagua viongozi wa wilaya watakuwa ni Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa matawi ya wilaya husika.

d) Kila Mkoa utafanya uchaguzi wa uongozi wake utakaohusisha Mwenyekiti wa Mkoa, Makamu Mwenyekiti wa Mkoa, Katibu Mkuu wa Mkoa, Mweka Hazina wa Mkoa na Wajumbe Watatu (3) (mmoja kati yao mjumbe mwanamke) ambao kwa ujumla wao ndio wataunda Kamati ya Utendaji ya Mkoa.

e) Mgombea wa nafasi yoyote ya Mkoa atatakiwa kuwa na sifa zifuatazo: -

(i) Awe na sifa zinazotakiwa kwa nafasi husika na amelipa ada ya uanachama kikamilifu tangu alipoanza uanachama.

(ii) Uanachama wake uwe ni kupitia moja ya tawi la Mkoa husika.

(iii) Awe na kiwango cha chini cha elimu ya angalau kidato cha nne.

(iv) Kiongozi wa kuchaguliwa atakaa madarakani kwa vipindi viwili tu vya kupiga kura kwa nafasi ya uongozi. Endapo atataka kurejea madarakani baada ya kutumikia vipindi viwili mfululizo, itabidi asubiri

kwanza kupita kwa walau uchaguzi mkuu mmoja wa kikatiba.

(v) Asiwe aliyewahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai kwa kuhukumiwa kifungo.

(vi) Awe na umri angalau miaka 25.

(vii) Asiwe mwamuzi wa mchezo wa Mpira wa miguu anayefanya shughuli za uamuzi kwa kipindi hicho.

f) Wapiga kura wa kuchagua viongozi wa Mkoa watakuwa ni Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa Wilaya za Mkoa husika.

g) Matawi yatawajibika kwa Uongozi wa kamati ya utendaji ya Wilaya, Uongozi wa Wilaya utawajibika katika Uongozi wa kamati ya utendaji ya Mkoa na Mkoa utawajibika katika Uongozi wa Bodi ya Wakurugenzi ya Makao Makuu.

h) Bodi ya Wakurugenzi itatengeneza kanuni za mahusiano na uendeshaaji wa uongozi wa Matawi, Wilaya na Mikoa, na pia kanuni za uchaguzi wa Matawi, Wilaya pamoja na Mikoa.

i) Uchaguzi wa Matawi, Wilaya na Mikoa utafanyika kila baada ya miaka minne, mwaka mmoja baada ya uchaguzi wa wajumbe wa SIMBA SPORTS CLUB kwenye Bodi ya wakurugenzi.

SEHEMU YA IV

FEDHA

Ibara ya 41: Mwaka wa Fedha

Mwaka wa Fedha wa SIMBA SPORTS CLUB utanza nautandana na Mwaka wa Fedha wa Simba Sports Club Company Limited.

Ibara ya 42: Mapato

Simba Sports Club itapata ruzuku ya kuendesha shughuli zake kutoka Simba Sports Club Company Limited.

Ibara ya 43: Matumizi

SIMBA SPORTS CLUB itakuwa na matumizi yafuatayo: -

- 1) Matumizi yaliyotajwa katika bajeti.
- 2) Matumizi mengine yaliyothibitishwa na Mkutano Mkuu na yale ambayo Bodi ya Wakurugenzi inastahiki kufanya ndani ya eneo la mamlaka yake.
- 3) Matumizi mengine yote kulingana na mipango na malengo ya SIMBA SPORTS CLUB.

SEHEMU YA V

MIPANGO BINAFSI

Ibara ya 44: Sheria za Michezo wa Mpira wa Miguu

SIMBA SPORTS CLUB itajiendesha kwa mujibu wa sheria na kanuni za mchezo wa Mpira wa Miguu zilizotangazwa rasmi na IFAB na Vyama vya Mpira TFF, CAF na FIFA.

Ibara ya 45: Mwenendo wa Viongozi na Vyombo wa Klabu

Vyombo na Viongozi wa SIMBA SPORTS CLUB lazima wafuate Katiba ya SIMBA SPORTS CLUB, Maamuzi na Kanuni za Maadili za Simba Sports Club Company Limited katika utendaji wa majukumu yao. Bodi ya Wakurugenzi itatayarisha Kanuni za maadili kwa kuzingatia Kanuni za Maadili za TFF.

Ibara ya 46: Kufukuzwa Uanachama

1. Bodi ya Wakurugenzi ndiyo yenye mamlaka ya kupeleka ajenda ya kufukuzwa uanachama kwenye Vyombo vya haki (Kamati ya Nidhamu au Kamati ya Maadili).
2. Vyombo vya Haki vitampa Mwanachama ambaye hoja ya kufukuzwa imepelekwa na Bodi ya Wakurugenzi nafasi ya kusikilizwa kwa kutumia kanuni zinazosimamia vyombo hivyo vya haki.
3. Mwanachama atakayefukuzwa lazima avuliwe majukumu yake mara moja.

Ibara ya 47: Migogoro ya Kisheria

Hairuhusiwi kutafuta msaada katika mahakama za kawaida za sheria dhidi ya maamuzi yaliyochukuliwa na vyombo vya SIMBA SPORTS CLUB na Simba Sports Club Company Limited. Maamuzi ya aina hiyo hayana budi kuwasilishwa katika Vyombo vya haki kwa mujibu wa Katiba ya

Simba, TFF na FIFA. Ukiukwaji wa kanuni hii utasababisha kufukuzwa uanachama kutoka SIMBA SPORTS CLUB.

Ibara ya 48: Leseni kwa Vilabu (Club Licensing)

SIMBA SPORTS CLUB itafata utaratibu wa TFF, CAF na FIFA juu ya utoaji wa leseni za Vilabu (Club Licensing System).

SEHEMU YA VI

MASHARTI YA MUDA NA MWISHO

Ibara ya 49: Mipango ya Utendaji

Bodi ya Wakurugenzi itahakikisha kuwa Katiba inatumika, na itapitisha mipango ya utendaji inayotakiwa kwa ajili ya kutumika.

Ibara ya 50: Masuala yasiyoelezwa katika Katiba

Suala lolote lisiloelezwa katika Katiba hii au kwa mambo yasiyozuilika, lazima yashughulikiwe na Bodi ya Wakurugenzi. Hakuna Rufaa itakayokatwa dhidi ya maamuzi yatakayotolewa na Bodi ya Wakurugenzi.

Ibara ya 51: Masharti ya Kutoa Huduma katika Kipindi cha Mpito

Jambo lolote litakalofanyika kabla na wakati wa kuanza kutumika kwa Katiba hii kuhusu kazi yoyote au jambo linaloweza kufanyika kwa mujibu wa Katiba hii litahesabiwa limefanyika kihalali kwa mujibu au kufuatana na Katiba hii.

Ibara ya 52: Kupitishwa na tarehe ya Kuanza kutumika

Katiba hii imepitishwa katika Mkutano wa Katiba wa SIMBA SPORTS CLUB tarehe 20/05/2018.

KWA AJILI NA KWA NIABA YA SIMBA SPORTS CLUB

SALIM ABDALLAH MHENE

KAIMU RAISI

HAMISI KISIWA

KAIMU KATIBU MKUU

KANUNI ZA MKUTANO MKUU

Ibara ya 1: Wajumbe

Wajumbe wa SIMBA SPORTS CLUB watajigharamia wenyewe usafiri, chakula na malazi wanaposhiriki kwenye Mkutano Mkuu isipokuwa kama itaamuliwa vinginevyo na Bodi ya Wakurugenzi. Bodi ya Wakurugenzi itatoa maagizo yanayofaa kuhusiana na hili.

Ibara ya 2: Mwenyekiti

- 1) Mwenyekiti ataongoza mkutano mkuu. Endapo Mwenyekiti hayupo au hawezi kuhudhuria, Bodi ya Wakurugenzi itamteua Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi inayeona anafaa kuongoza Mkutano Mkuu.
- 2) Mwenyekiti atahakikisha Mkutano Mkuu unaendeshwa kwa kufuata na kutii kanuni kuu, kufungua na kufunga Mkutano Mkuu na mijadala, na kuwapa wajumbe ruhusa ya kuzungumza na kuendesha majadiliano yote.
- 3) Mwenyekiti atakuwa na jukumu la kuhakikisha utulivu na utaratibu wakati wa mijadala. Anaweza kuchukua hatua zifuatazo dhidi ya mwanachama yeyote wa Mkutano Mkuu anayesumbua majadiliano:
 - a) Kuomba utulivu
 - b) Karipio
 - c) Kusimamishwa kikao kimoja au zaidi
- 4) Iwapo Rufaa itaombwa dhidi ya hatua hiyo, Mkutano Mkuu utaamua mara moja bila ya mjadala.

Ibara ya 3: Wasimamizi

Kabla ya kuanza Kikao, Mkutano Mkuu utateua idadi ya kutosha ya wasimamizi ili kuhesabu kura. Bodi ya Wakurugenzi inaweza kutumia kifaa cha elektroniki kuamua matokeo ya kura.

Ibara ya 4: Wakalimani

Wakalimani rasmi watateuliwa na Mkutano mkuu kufasiri lugha rasmi ya Mkutano Mkuu.

Ibara ya 5: Mijadala

Mijadala kwa kila dondoo la ajenda itafuatiwa na taarifa fupi itakayotolewa na:

- 1) Mwenyekiti au Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi aliyeteuliwa kwaajili hiyo.
- 2) Mwakilishi wa Kamati aliyeteuliwa na Bodi ya Wakurugenzi Kutoa taarifa.
- 3) Mjumbe aliyeomba dondoo liingizwe katika agenda
- 4) Kisha Mwenyekiti atafungua mjadala

Ibara ya 6: Mzungumzaji

- 1) Ruhusa ya kuzungumza inatolewa kwa utaratibu na mfuatano wa maombi. Mzungumzaji hawezi kuanza kuzungumza mpaka aruhusiwe kufanya hivyo.
- 2) Mzungumzaji hawezi kuzungumza mara ya pili katika dondoo moja mpaka wajumbe wote walioomba kuchangia mwanzo wamalizike.

Ibara ya 7: mapendekezo

- 1) Mapendekezo yote yatawasilishwa kwa maandishi. Mapendekezo yasiyo muhimu kwa mada inayojadiliwa hayataruhusiwa kuingia katika mjadala.
- 2) Marekebisho yoyote yataandikwa na kupelekwa kwa Mwenyekiti kabla ya kuingizwa katika mjadala.

Ibara ya 8: Hoja za Utaratibu wa kufunga Mjadala

- 1) Iwapo hoja ya utaratibu imetolewa, majadiliano kuhusu mada kuu yatasimama mpaka kura ipigwe kuhusu hoja.

- 2) Iwapo hoja imetolewa ya kufunga majadiliano itapigiwa kura mara moja bila majadala. Iwapo hoja inathibitishwa idhini ya kuzungumza itatolewa tu kwa wajumbe walioomba kuzungumza kabla ya kura kupigwa.
- 3) Mwenyekiti atafunga majadiliano isipokuwa kama Mkutano Mkuu utaamua vingine kwa wingi mdogo wa kura ya wale wanaopiga kura.

Ibara ya 9: kura

1. Upigaji kura ya siri umekatazwa, isipokuwa kwa uchaguzi.
2. Kabla ya kila Kura, Mwenyekiti au Mwanachama aliyeteuliwa na Mwenyekiti, atasoma pendekezo kwa sauti na kueleza utaratibu wa kupiga kura na akidi kwa Mkutano Mkuu.
3. Kura inaweza kupigwa kwa kusoma majina iwapo imeombwa na wingi wa wanachama waliohudhuria na wenye haki ya kupiga kura.
4. Hakuna anayelazimishwa kupiga kura.
5. Kura zitapigwa kwa kunyoosha mikono (kadi za kura) au kwa kutumia kifaa cha elektroniki.
6. Mapendekezo yatapigiwa kura kwa mfuatano wa jinsi yalivyowasilishwa iwapo kama kuna zaidi ya mapendekezo mawili makuu, yatapigiwa kura kwa mfuatano, na wajumbe hawataruhusiwa kupigia kura zaidi ya pendekezo moja.
7. Mabadiliko katika marekebisho yatapelekwa kwenye Mkutano Mkuu kabla ya marekebisho yenyewe na marekebisho kabla ya mapendekezo Makuu.
8. Mapendekezo yasiyo na kura ya kupinga, yanahesabiwa kuwa yamepita.

9. Mwenyekiti atahakikisha matokeo ya kura na kuyatangaza katika Mkutano Mkuu.
10. Hakuna mjumbe anayeruhusiwa kuzungumza wakati wa kupiga kura mpaka baada ya matokeo kutangazwa.
11. Ili mgombea aweze kupewa Fomu ya kugombea atalazimika kulipa ada iliyopendekezwa na Kamati ya Uchaguzi kwenye Klabu ya SIMBA SPORTS CLUB na kupewa stakabadhi ambayo ataonyesha kwa Msimamizi wa Uchaguzi, kabla ya kupewa fomu ya kugombea uongozi.

KWA AJILI NA KWA NIABA YA SIMBA SPORTS CLUB

SALIM ABDALLAH MHENE

KAIMU RAISI

HAMISI KISIWA

KAIMU KATIBU MKUU